



P. O. Box 9968,
Plot No. 4. Keko,
M: +255 715 253 653
E: tpbrctz@gmail.com,
W: www.tpbrctz.org.tz
Dar es Salaam,
Tanzania,
East Africa.

TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI

KAMATI ya Sheria, Nidhamu, Utatuzi na Usuluhishi wa Migogoro ya Kamisheni ya Kusimamia Ngumi za Kulipwa nchini Tanzania katika kikao chake cha tarehe 14-01-2023 ilisikiliza malalamiko ya promota Shomari Kimbau dhidi ya ndugu Bakari Songoro, Abdallah S. Pazzy *almaarufu* Dulla Mbabe na Ali Mwazoa mwenye umiliki wa Mwazoa Promotion Boxing, kuwa promota Shomari Kimbau analalamika dhidi ya walalamikiwa hao kuwa na nia ovu ya kumuharibia pambano lake la tarehe 27-01-2023 linalotarajiwa kufanyika Zanzibar. Kamati iliamua kama ifuatavyo: -

Kwamba, suala hilo limekaa kimkataba zaidi kwa maana msingi wa malalamiko ya promota Shomari Kimbau hayakuwa na mashiko mbele ya Kamati hiyo kwa maana utaratibu wa kuleta malalamiko yake haukupaswa kuletwa mbele ya Kamati hiyo kwa sababu malalamiko yake yalikuwa na mapungufu mengi ya kimkataba dhidi ya ndugu Bakari Songoro, Abdallah S. Pazzy *almaarufu* Dulla Mbabe na Ali Mwazoa, huku malalamiko hayo yamekuwa na maudhui zaidi ya kesi ya madai jambo ambalo linapaswa kupelekwa kunako vyombo vyenye dhamana ya kusimamia haki mathalani Mahakama kuliko kuwasilisha kwenye Kamati tajwa.

Hivyo, Kamati imempa nafasi promota Shomari Kimbau kuona namna bora ya kuwasilisha jambo lake kwa njia iliyo sahihi zaidi kuliko hiyo aliyoitumia


Yahya Poli

Katibu

16 January, 2023

